

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI
WIZARA YA ELIMU SAYANSI TECHNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA**

Shule ya sekondari Mwandete,
S.L.P 349,
MASWA - SIMIYU
09/12/20.....

Kumb. Na MoESTVT/S.1702/J.I/...../.....

Mwanafunzi.....
S.L.P.....
MASWA.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWANDETE
20.....**

1. UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mwandete baada ya kuhitimu na kufaulu vizuri elimu ya msingi mwaka 20..... shule hii ipo katika Wilaya ya Maswa mkoa wa Simiyu kutoka njia kuu ya Maswa Meatu kilomita 01 kusini mwa barabara uteremkia Mwandete madukani. Shule hii niya kutwa hivyo utakuwa ukija shule na kurudi nyumbani. Shule hii imejengwa kwa nguvu za wananchi wa kata mbili Dakama na Sangamwalugesha. Hivyo nimatumaini yetu kuwa utayatunza vizuri majengo na samani zake. Shule itafunguliwa siku ya juma tatu tarehe...../01/20.....

Kabla hujaripo kamilisha ujazaji wa fomu mbili zifuatazo na uje nazo siku ya kuripoti shule.

I. CHETI CHA HOSPITALI (STUDENTS MEDICAL CERTIFICATE FORM "A"

Fomu hii iijazwe na dactari wa hospitali ya serikali na siyo hospitali binafsi. Endapo unamatatizo ya kiafya ni vizuri umtaarifu dactari ili akuchunguze na kukupa ushauri. Fika na fomu hii siku ya kuripoti ikiwa imejazwa na imegongwa mhuri na dactari.

II. MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI KUHUSU AHADI ZA UTII FOMU "B"

Soma fomu hii kwa uangalifu kisha iijazwe na kuthibitishwa na Mwanafunzi pia na Mzazi sehemu yake. Fomu hii irudishwe siku ya kuripoti shulenii bila kukosa. Mzazi fika na mwanao bila kukosa vinginevyo hatutampokea mwanafunzi ambaye ataletwa na mtu ambaye siyo mzazi au mlezi. Mzazi timiza wajibu wako kwa kumnunulia mwanao vifaa na mahitaji ya shule yote uliyoainishiwa hapo chini.

- Begi la madaftari
- Daftari 10 kubwa
- Kalamu za biki 03
- Rula 01
- Penseli 01
- Ufutio
- Ufagio wa chelea wenye ushikio wa mti kwa ajili ya usafi wa mazingira.

2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) wizi (ii) uasherati (iii)ubakaji (iv)kupigana au kupiga (v) kudharau bendera ya Taifa (vi)ulevi na matumizi ya madawa ya levya na pombe (vii) kuharibu mali za shule kwa makusudi (viii) kuoa au kuolewa (ix) kupata mimba/kumpa mimba mwanafunzi (x) kutoa mimba (xi)kukataa adhabu kwa makusudi (xii)kugoma au kuchochea mgomo (xiii)kumiliki simu ya mkononi (xiv) utoro zaidi ya siku 90 (xv) uzembe darasani.

3. SARE ZA SHULE.

A: Mavazi rasmi darasani:-

i. **Wasichana.**

- a) Sketi za rangi nyeusi mbili za kitambaa kizito cha suti namba moja. Sketi hizi ziwe ndefu usawa wa soksi zinapoishia zinapokuwa zimevaliwa.
- b) Shati mbili za tetro za mikono mifupi inayoishia kwenye kiwiko cha mkono ambazo si za kubana, wala kuonyesha nguo za ndani. Pia mzazi kumbuka kumnunulilia mwanao blauzi mbili nyeupe kwa ajili ya kuvalia shati za shule.
- c) Viatu vyeusi vya ngozi pea mbili vya kufunika miguu visivyo na urembo wowote.
- d) Soksi nyeupe ndefu pea mbili.
- e) Tai mbili nyeusi na ndefu usawa wa sketi.

ii. **Wavulana:**

- a) Suruali mbili za rangi nyeusi za kitambaa kizito cha suti namba moja na si za jinzi/dengilizi. Zisiwe za kubana (modo).
- b) Shati mbili nyeupe za tetro za mikono mifupi inayoishia kwenye viwiko. Pamoja na flana mbili nyeupe kwa ajili ya kuvalia shati la shule.
- c) Viatu vyeusi vya ngozi pea mbili vyakufunga na kamba, visiwe raba wala aina nyingine.
- d) Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
- e) Tai mbili nyeusi na ndefu zinazofika usawa wa mkanda wa suluwali

Mtoto akija shule na mavazi hayaendani na maelekezo hapo juu hata pokelewa.

NB: Kumbuka kuchomekea shati ndani ya sketi au suruwali muda wote uwapo katika vazi la shule kwani ni sheria ya shule.

B: Mavazi ya kazi na michezo.

i. **Wasichana.**

- a) Tisheti ya rangi ya bluu nyeusi
- b) Viatu vya raba vyenye njumu rangi yoyote
- c) Traka suti ya bluu kwa ajili ya michezo

ii. **Wavulana.**

- a) Tishati ya rangi ya bluu nyeusi
- b) Viatu vya raba vyenye njumu rangi yoyote
- c) Traka suti ya bluu kwa ajili ya michezo

4. SHERIA ZA SHULE.

Kila Mwanafunzi anatakiwa kutii sheria za shule pamoja na taratibu zingine za shule kadri zitakavyotolewa na uongozi wa shule. Sheria hizi utazikuta zimebandikwa kwenye mbao za matangazo za shule na madarasani.

Ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kutofahamu **SHERIA ZA SHULE**

5. MWISHO.

Nimatumaini yangu kuwa utaipokea nafasi hii ya pekee kwa furaha kubwa na hautaipoteza.

Nakutakia maandalizi mema.

KUMBUKA
"ELIMU KWA MABADILIKO BORA"
KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MWANDETE

WAKO,

.....
FRANCISCO E. BUJIKU